JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA
SHULE YA SEKONDARI AZANIA

Simu: +255 719 999 830
Barua pepe :info@azaniasecondary.sc.tz
headmaster@azaniasecondary.sc.tz
Tovuti : http://www.azaniasecondary.sc.tz

Ofisi ya Mkuu wa Shule,
S.L.P 9074,
Dar es salaam.
Upanga Magharibi

Kumb. Na. AZ/F5/_____ Tarehe .....

KWA MZAZI / MLEZI WA ----------

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI AZANIA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA MKOA WA DAR ES SALAAM
KIDATO CHA TANO HADI CHA SITA MWAKA 2017/18

1. UTANGULINZI:
Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao **AMECHAGULIWA /AMEHAMISHIWA** Shule ya Sekondari Azania kidato cha Tano/Sita mwaka _____Tahasusi ya ECA [ ] EGM [ ] PCB [ ] na PCM [ ] .Shule ya Sekondari Azania ni ya **Kutwa. HONGERA NA KARIBU SANA.**

2. MAHALI SHULE ILIPO:
Shule hii ipo katika Barabara ya Umoja wa Mataifa karibu na kituo cha **ZIMAMOTO** (**FIRE**) **KATI YA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA JANGWANI NA** Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

3. MUHIMU
Muhula wa masomo unaanza tarehe **03/07/2017**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti tarehe **05/07/2017 akiwa na Matokeo yake ya kidato cha Nne (Result Slip) Bila hiyo hatapokelewa.**.Mwisho wa kuripoti mwanafunzi ni tarehe **17/07/2017** baada ya tarehe hiyo **HATAPOKELEWA.**

4. MAHITAJI YA SHULE.
A. (i) Sare ya shule ni **Suruali ya rangi ya "Dark Green"** na **Shati jeupe la mikono mifupi (tomato) na Tai yenye rangi ya suruali**. Unatakiwa kuwa na jozi moja ya Suruali ambayo itapatikana hapa shuleni.
(ii) **Viatu vyeusi vya ngozi visivyochongoka**,vya kamba, siyo raba.
(iii) **Soksi nyeusi** jozi moja
(iv) **Mkanda mweusi** wa ngozi wenye kichuma cha kawaida cha Kufungia suruali.
(v) **Sweta moja** lenye rangi ya Suruali.

B. 1. MAHITAJI KWA WALIOCHAGULIWA KUKAA BWENI TU:

(i) Godoro la futi 2 ½ x 6 (lenye kitambaa)
(ii) Shuka mbili (2) futi 4 x 6 (light blue)
(iii) Chandarua futi 4 x 6 (cheupe)
(iv) Taulo na sanduku la bati (kuhifadhi nguo)
(v) Nguo za Kushindia ni T-shirt 2 za rangi ya Kijivu na Blue Bahari ambazo zitavaliwa muda wote awapo Bwenini (**Zinapatikana hapa shuleni).**

2. VIFAA VYA CHAKULA:

(i) Sahani.
(ii) Kijiko.
(iii) Bakuli na Kikombe cha ½ lita.

3. VIFAA VYA USAFI:

(i) Ndoo ndogo mbili(2) za lita 10 (Plastiki)
(ii) Vifaa vingine vyote muhimu mfano: Sabuni za kuogea na kufulia za Kutosha, Mswaki, Dawa ya Meno n.k.

"ANGALIZO": Ni marufuku kwa mwanafunzi kuja na vitu vya thamani kama **Redio, TV, Laptop, Simu** n.k.

C. MAHITAJI MENGINE YA MWANAFUNZI:

(i) Madaftari makubwa (**Counter Books**)
(ii) Mathematics Set na Calculator (Scientific Calculator).
(iii) Kalamu za Wino na Penseli za kutosha.
(iv) Rula na kifutio.
(v) Rimu moja ya karatasi za Photocopy .
(vi) Vitabu vya masomo ya Tahasusi husika (pata ushauri toka kwa mwalimu/Idara husika), mfano somo la Biology;
- **Biological science 3rd Ed. 2011 by D. J. Tayler N.P.O. Green and G.W. Staut**
– **Guide to dissection by HGQ Rowett, M.A., and M. I. Biology.**

(vii) Dissection Kit Kwa wanafunzi wa Somo la Biology.
(viii) **Kwanja/Jembe/Reki moja na Mifagio miwili:ndani na nje.**
(ix) Begi la kubebea vifaa vyake.

ANGALIZO: Kila Tahasusi itapangiwa kifaa cha kuleta ajapo shule.

5. A. KARO NA MICHANGO YA SHULE

Ada ya shule kwa mwaka ni **Tsh.20, 000** kwa mwanafunzi wa kutwa na **Tsh.70,000** kwa mwanafunzi wa bweni.Unaweza kulipa kiasi cha Tsh.10,0000 kwa wanafunzi wa kutwa na Tsh.35,000 kwa mwanafunzi wa bweni kwa muhula au kulipa ada yote kwa maramoja.Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunt ya Shule **Na.2031100094** katika benki ya **NMB.(**Tafadhali andika Jina la mwanafunzi kwenye Pay in slip).Malipo yanayotakiwa ni ya mwaka huu tu.

B. MICHANGO INAYOTAKIWA KULIPWA NA KILA MZAZI.

i) Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa Samani.Fedha hii ilipwe kwenye akaunti **Na:2031100154** katka benki ya **NMB.**
ii) Shilingi 6.000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha.
iii) Shilingi 20,000 /= kwa ajili ya taaluma.
iv) Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi,Walinzi na vibarua wengine.
v) Shillingi 2,000/= nembo ya shule.
vi) Shilingi 10,000/= : Tsh.5,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza, na Tsh.5,000/= Bima ya afya (wanafunzi mnashauriwa kujiunga na mfuko wa Bima ya Afya **-CHF**).
vii) Shilingi 20,000/= mitihani ya kujipima(Mock).
viii)Fedha ya Tahadhari ni Shilingi 5,000/=(haitarejeshwa).
ix) Shilingi 10,000/= kwa ajili ya kunyonya Maji taka.(Kwa Wanaokaa bweni tu).

6. RATIBA YA SHULE huanza **Saa 1.00 asubuhi** hadi **saa 8.30 mchana**.

NB: RATIBA YA SIKU ZA IJUMAA huanza saa 1.00 asubuhi na kuishia **saa 6.00 mchana** ili kuwawezesha **Wanafunzi wa Kiislamu** kuhudhuria **SWALA YA IJUMAA.** Pia Lugha ya mazungumzo awapo mazingira ya shule ni **KISWAHILI NA KIINGEREZA.**

7. KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE:

A. MAHUDHURIO:

Mwanafunzi hana budi kuhudhuria vipindi vyote vya masomo Darasani na siku za masomo kwa mwaka (siku 196) . Mwanafunzi atakayeshindwa kuhudhuria **MBILI YA TATU (2/3**) ya siku hizo **BILA SABABU MAALUMU** atakuwa **AMEJIONDOA** mwenyewe shuleni.

B. SHERIA ZA SHULE:

i) Sare zivaliwe – shati lichomekewe ndani ya suruali, na kufunga mkanda mweusi.
ii) Shati lazima liwe na **NEMBO** ya shule Kila siku.
iii) Nywele ziwe fupi- mkato wa kawaida bila mtindo wowote; bwenzi, kipara haviruhusiwi.
iv) Mwanafunzi hana budi kuwaheshimu au kuwatii watu wote, walimu, wafanyakazi wasio walimu,viongozi na wageni wanaofika Shuleni.
v) Kuvaa pete, bangili, mkufu au marembo yoyote hayaruhusiwi.
vi) Epuka vitendo viovu kama **matusi, utoro, wizi, ugomvi, ulevi na pombe, madawa ya kulevya, uvutaji sigara, bangi, uasherati ; ushoga, kuoa, kuchochea migomo na vitu** vinginevyo. Kwani makosa haya yanaweza kumfanya mwanafunzi achukuliwe hatua zilizotajwa hapa chini (Kipengele **8** au **9**).
vii) Timiza wajibu wa **kazi** uliyopangiwa.
viii)Usiandike mahali pasipohusika kama vile kutani, vitabuni, kwenye samani nk.
ix) Usimpige au kumshambulia mwanafunzi mwenzako au hata mtu mwingine yeyote.
x) Usifanye biashara yoyote shuleni

xi) Usibandike tangazo lolote bila ruhusa ya mwalimu anayehusika na kukilea kikundi kinachohusika.
xii) Usikatae uteuzi wa kushiriki shughuli mbalimbali kama vile michezo, maandamano, uwakilishi n.k.
xiii) Usihubiri dini, siasa au jambo lolote. Sala zote zifanyike mahali panapohusika kama vile **Kanisani** au **Msikitini.**

C. HATUA ZICHUKULIWAZO KWA KUKIUKA TARATIBU NA SHERIA ZA SHULE:

(i) Kuonywa
(ii) Kufanyakazi za mikono zaidi
(iii) Kuchapwa viboko
(iv) Kusimamishwa Shule

D. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE:

i) Wizi
ii) Uasherati
iii) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
iv) Uvutaji bangi.
v) Makosa ya Jinai.
vi) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
vii) Kupigana au kupiga.
viii) Kuoa au Ushoga.
ix) Kudharau Bendera ya Taifa.
x) Kusababisha **mimba.**
xi) Kusaidia kutoa mimba.
xii) Kukataa adhabu kwa makusudi
xiii) Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani au usalama wa Shule au watu.
Xiv) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu.
xv) Kushiriki vitendo vya ugaidi.
xvi) Utoro.
xvii) Kutofanya Mitihani bila sababu.

8. ULINZI WA MALI ZA SHULE NA BINAFSI:

Mwanafunzi lazima awe mlinzi na mtunzaji wa mali zote za Shule na za binafsi.

9. MENGINEYO:

Ni **marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu** ya kiganjani akiwa ndani au nje ya darasa. Atakayepatikana na simu adhabu kali itachukuliwa dhidi yake **sanjari na kunyang'anywa hiyo simu** na **KUHARIBIWA papo hapo.**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI AZANIA

NAKALA KWA:

: Afisaelimu Wilaya.
: Afisa Elimu wa Mkoa.
: Mkaguzi Mkuu – Kanda ya Dar es salaam.

HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA
SHULE YA SEKONDARI AZANIA

Simu: +255 719 999 830
Barua pepe :info@azaniasecondary.sc.tz
headmaster@azaniasecondary.sc.tz
Tovuti : http://www.azaniasecondary.sc.tz

Ofisi ya Mkuu wa Shule,
S.L.P 9074,
Dar es salaam.
Upanga Magharibi

Kumb. Na. AZ/F5/_____ Tarehe .....

YAH: FOMU YA USAJILI (IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI).

PICHA YA MWANAFUNZI

SEHEMU "A" IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE.

Jina kamili la Mwanafunzi _____
Tarehe ya kuzaliwa_____ (3) Mahali (Wilaya) _____
(4) Uraia _____ (5) Dini_____Dhehebu_____
(6) Shule ya Msingi uliyosoma_____
Namba ya Mtihani PS. _____
(7) Shule ya Sekondari uliyopangwa (FI - IV) _____
(8) Shule ya sekondari uliyotoka (FV) _____
Nambari ya Mtihani S._____
(9) Mahali unapoishi kwa sasa _____

AHADI YA MWANAFUNZI:

Mimi _____ Nakubali nafasi niliyopewa ya Kidato cha **Kwanza / Pili /Tatu / Nne / Tano.**

Naahidi kutii kikamilifu Sheria / Kanuni zote za shule wakati wote niwapo mwanafunzi wa **AZANIA.**

SAHIHI YA MWANAFUNZI_____**TAREHE**_____

SEHEMU B: IJAZWE NA MZAZI / MLEZI:

PICHA YA MZAZI / MLEZI

1. Jina la Mzazi/Mlezi _____
2. Kazi _____
3. Anuani _____
4. Simu _____
5. Mahali ninapoishi_____

AHADI YA MZAZI / MLEZI YA KULIPA KARO / MICHANGO YA SHULE:

Mimi_____Mzazi /Mlezi wa _____ wa **Kidato cha Kwanza/Pili /Tatu / Nne /Tano mwaka 20**_____ katika **Shule ya sekondari AZANIA**. Nathibitisha na kuahidi kuwa nipo tayari kulipa **KARO** ya **TSHS 20,000** kwa mwaka pamoja na michango mingine inayoidhinishwa na shule au mamlaka ya elimu kwa ajili ya maendeleo ya shule na wanafunzi.

Pia naahidi kuwa kila ifikapo mwisho wa **Muhula wa Shule** (**Mwezi Juni** au **Desemba**) Nitakuwa nimemamiliza deni kwa mwaka huo. **Karo / Mchango** utalipwa na **Ndugu**_____ **wa S.L.P.**_____ **Simu namba** _____

SAINI YA MZAZI/ MLEZI_____ **TAREHE**_____

HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA
SHULE YA SEKONDARI AZANIA

Simu: +255 719 999 830
Barua pepe :info@azaniasecondary.sc.tz
headmaster@azaniasecondary.sc.tz
Tovuti : http://www.azaniasecondary.sc.tz

Ofisi ya Mkuu wa Shule,
S.L.P 9074,
Dar es salaam.
Upanga Magharibi

Kumb. Na. AZ/F5/_____ Tarehe .....

FOMU NA 2: FOMU YA TAARIFA YA AFYA YA MWANAFUNZI
"MEDICAL EXAMINATION FORM"

Maelezo: Fomu hii ijazwe na Mganga Mkuu wa Mkoa /Wilaya / Kituo cha Afya na Mwanafunzi aje nayo shuleni na kuikabidhi ofisi ya nyaraka za wanafunzi.

Mimi [Jina la Mganga Mkuu wa Mkoa/Wilaya]_____
Nathibitisha kuwa Mwanafunzi [Jina la mwanafunzi]_____
Amepimwa nami kikamilifu na kuonekana anayo / hanayo afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo;-

[A] **Hali ya mwili**

[I] Mapigo ya moyo_____
[ii] Haemoglobin;_____
[iii] Kundi la damu [blood group]_____
[iii] Mkojo (Urine) _____
[iv] Kinyesi (Stool) _____
[vi] Macho yana kasoro_____
[vii] Masikio yana kasoro_____

Angalia: Weka maoni yako kuhusu kila kilichotajwa (a) (**i**) - (**vii**)

[B] **Magonjwa**

[a] Bronchial asthma_____
[b] Tuberculosis_____
[c] Epilepsy_____
[d] Blood pressure_____
[e] Peptic/duodenal ulcers_____
[f] Sickle cells_____
[g] Leprosy _____
[h] Venereal disease [give type]_____
[I] Mental illness_____
[j] Any other serious disease not mentioned above

Saini ya Daktari _____ **Tarehe**_____ **Muhuri**

Futa neno lisilo husika